# BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

70 Barabara yaChukwani, Buyu,
70490 MjiniMagharibi,
S.L.P 902 Chukwani,
Zanzibar, Tanzania

Simu: +255 24 224 2000
Nukushi: +255 24 2242000
info@zanzibarassembly.go.tz
www.zanzibarassembly.go.tz

**HOTUBA YA MWENYEKITI WA KAMATI YA UTALII, BIASHARA NA KILIMO YA BARAZA LA WAWAKILISHI KUHUSU MSWADA WA SHERIA YA KUFUTA SHERIA YA MAMLAKA YA KUKUZA NA KULINDA UWEKEZAJI ZANZIBAR, NAM. 14 YA 2018 NA KUTUNGA SHERIA YA UWEKEZAJI ZANZIBAR NA KUWEKA MASHARTI MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO.**

**Mheshimiwa Spika,**

Naanza hotuba hii kwa kumshukuru Mola Mtukufu, aliyetujaalia uzima na afya njema na kutuwezesha kukutana leo hii ndani ya Baraza lako Tukufu kuendelea na majukumu yetu ya Kitaifa. Namuomba Mwenyezi Mungu anijaaliye ufasaha katika uwasilishaji wa Hotuba hii na atupe usikivu na uelewa ili hatimaye tuweze kuuchangia kwa umakini mswada uliopo mbele yetu kwa maslahi mapana ya nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika,**

Napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kuniruhusu kusimama mbele ya Baraza lako Tukufu ili niwasilishe maoni ya Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo kuhusiana na "Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria Ya Mamlaka Ya Kukuza na Kulinda Uwekezaji Zanzibar, Nam. 14 Ya 2018 na Kutunga Sheria ya Uwekezaji Zanzibar na Kuweka Masharti Mengine Yanayohusiana na hayo".

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa namna ya pekee nachukua fursa hii kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa jitihada anazochukua za kuendeleza sekta ya Uwekezaji ambayo ni sekta inayoinukia nchini na kuleta mwanga wa ukuwaji wa uchumi wa nchi yetu.

Kadhalika, napenda kuwapongeza Makamu wa Kwanza na Makamu wa Pili wa Rais kwa msaada mkubwa wanaompatia Mheshimiwa Rais katika utekelezaji wa jukumu la uongozi wa nchi yetu. Namuomba mwenyezi Mungu awajaaliye afya njema na maisha marefu viongozi wetu ili tuzidi kuneemeka kwa uongozi wao bora.

**Mheshimiwa Spika,**

Naomba kutumia fursa hii kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Mudrik Ramadhan Soraga, (Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais Kazi, Uchumi na Uwekezaji), Makatibu wakuu, Naibu makatibu wakuu pamoja na jopo la watalaamu wao kwa mashirikiano waliyoipatia Kamati yetu katika kipindi chote cha majadiliano ya Mswada huu.

Kadhalika, napenda kuwashukuru Wanasheria wa Afisi ya Baraza la Wawakilishi pamoja na Wanasheria kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (AG) kwa uchambuzi na ufafanuzi wa hoja mbali mbali zilizojitokeza wakati wa kuujadili mswada huu kwenye ngazi ya Kamati. Ni dhahiri kuwa, hoja zote zilizoibuliwa na Kamati yetu zililenga kuujenga zaidi mswada huu kwa maslahi ya Taifa letu.

**Mheshimiwa Spika,**

Nawapongeza kwa dhati Waheshimiwa Wajumbe wenzangu wa Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo kwa kazi nzuri waliyoifanya katika kupitia mswada

huu wa sheria ya Kufuta Sheria Ya Mamlaka Ya Kukuza na Kulinda Uwekezaji Zanzibar, Nam. 14 Ya 2018 na Kutunga Sheria ya Uwekezaji Zanzibar na Kuweka Masharti Mengine Yanayohusiana na hayo". Naomba kuwatambulisha Wajumbe hao pamoja na makatibu wao kwa majina kama ifuatavyo:

1. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf - Mwenyekiti
2. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu - M/Mwenyekiti
3. Mhe. Said Saleh Salim - Mjumbe
4. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa - Mjumbe
5. Mhe. Mihayo Juma Suleiman - Mjumbe
6. Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis - Mjumbe
7. Mhe. Suleiman Makame Ali - Mjumbe
8. Ndg. Abubakar Mahmoud Iddi - Katibu
9. Ndg. Yussuf Mkamba Mwinyi - Katibu
10. Ndg. Asma Ali Kassim - Katibu

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati yetu imeupitia kwa makini mswada wa sheria ya Kutunga Sheria ya Uwekezaji Zanzibar, 2023 na kufanya marekebisho madogo madogo kwa nia ya kuuimarisha zaidi. Marekebisho hayo yamehusisha makosa ya kiuandishi, kuingiza maneno yaliyokosekana ili kukamilisha maana, kuingiza vifungu vipya pamoja na kuingiza baadhi ya maneno ili kuleta upatanisho baina ya nakala ya Kiswahili na ya Kiingereza.

**Mheshimiwa Spika,**

Vifungu kadhaa vya mswada huu vinahitaji uwepo wa kanuni ili kuweza kutekelezeka vikiwemo kifungu cha 8, 51 na 56. Hivyo, tunamshauri Mheshimiwa Waziri kutunga kanuni hizo mapema iwezekanavyo ili sheria hii iweze kutekelezeka mara tu baada ya kutiwa saini na Mheshimiwa Rais.

**Mheshimiwa Spika,**

Ardhi ni rasilimali muhimu katika kukuza na kuendeleza sekta ya uwekezaji nchini. Kwa kutambua hilo, Serikali imeiweka rasilimali hiyo chini ya umiliki wake ili kufanya matumizi sahihi kwa maslahi mapana ya Taifa. Kamati yetu inaunga mkono dhamira ya kifungu cha (7) kifungu kidogo ( e) cha mswada huu ambacho kinaipa fursa Mamlaka ya Uwekezaji kukodisha ardhi na kutoa hati ya ardhi kwa mwekezaji katika maeneo maalum ya uchumi. Jambo hili litarahisisha upatikanaji wa ardhi kwa wawekezaji wa ndani na nje ya nchi ili kuendeleza shughuli walizojipangia kwa wakati na kuifungua Zanzibar kiuchumi kupitia sekta hii ya Uwekezaji.

**Mheshimiwa Spika,**

Katika kifungu cha 9 kinachohusu uanzishwaji na muundo wa Bodi, Kamati inapendekeza kuingizwa mjumbe mmoja kutoka Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA) awe ni sehemu ya wajumbe wa bodi ya Mamlaka ya Uwekezaji ili kujuwa mwelekeo sahihi wa uwekezaji nchini na kuweka sera zinazofaa kwa ukuzaji wa mapato ya Nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika,**

Uongozi makini (ambao hupatikana kutokana na uzalendo, ujuzi na weledi wa kiongozi aliyeteuliwa) ndio chachu ya maendeleo Taasisi inayokusudiwa kuundwa kupitia Sheria hii. Kwa msingi huo, Kamati inapendekeza kufanyiwa marekebisho kifungu cha 10 cha mswada huu kwa kuongeza sifa ya ziada ya Mwenyekiti wa Bodi kuwa “awe ni Mtanzania” ili kuzingatia kwa upana wake Maslahi ya Wazawa katika sekta nzima ya uwekezaji nchini.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati yetu inapendekeza kufutwa kwa kifungu cha 42 kifungu kidogo cha (3) na kuandikwa upya kisomeke " **Mamlaka itabakiza asilimia mia moja (100) ya fedha zilizokusanywa**". Hatua hii ni muhimu katika kuipa nguvu Mamlaka ya Uwekezaji kutekeleza shughuli zake za msingi kwa ufanisi.

**Mheshimiwa Spika,**

Kifungu cha 33 kinachohusu ushirikishwaji wa wazawa na wajibu wa kijamii kinapendekezwa kufutwa na kuandikwa upya kisomeke "**Mwekezaji atafuata miongozo ya mazingira,jamii na utawala iliotolewa chini ya masharti ya Sheria hii"**

Marekebisho hayo yanayopendekezwa na Kamati yetu yanalenga kuakisi dhana ya utunzaji wa mazingira na wajibu wa kijamii kwa upana wake kwa mwekezaji takayeekeza nchini.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati yetu inakubaliana na kifungu cha 37 cha mswada huu kinachohusu ajira kwa Watanzania na kusisitiza utekelezwaji wake kivitendo mara tu sheria hii itakapoanza kutumika kutokana na ukweli kwamba, Zanzibar ni sehemu ndogo na ina wajibu wa kulinda fursa chache ilizonazo kwa ajili ya vijana wake, ili kukabiliana na ukosefu wa ajira na kufikia malengo yetu ya kuzalisha ajira 3000 ifikapo mwaka 2025.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inapendekeza kufanywa marekebisho katika kifungu cha 3 (c ) cha Sehemu ya tatu ya Jadweli la tano kwa kufuta neno "**mitano**" lililopo baina ya neno "**miaka**" na "**ya kwanza**" na kuandika neno "**kumi**" ili kuakisi maana halisi ilyokusudiwa na kuleta uwiano baina ya mswada wa kiingereza na wa Kiswahili.

**Mheshimiwa Spika,**

Marekebisho mengine yaliyopendekezwa na Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo yameainishwa kwenye waraka wa marekebisho ambao tayari umeingizwa kwenye mfumo wa Baraza mtandao.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa kumalizia, natoa shukurani za dhati kwa Wajumbe wote wa Baraza lako Tukufu kwa utulivu na usikivu wao wakati wote wa uwasilishaji wa taarifa yetu na naomba tuuchangie, tuujadili, tutowe mapendekezo na hatimae tuupitishe mswada huu ili kuimarisha uwekezaji utakaoleta tija kwa jamii.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa niaba ya Kamati yangu, naomba kuwasilisha.

……………………

Mhe. Mtumwa Peya Yussuf,
Mwenyekiti,
Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo,
Baraza la Wawakilishi,
**Zanzibar.**